OSHA
Occupational Safety and Health Authority
JARIDA MTANDAONI
TOLEO MAALUM LA MWEZI JUNI NA JULAI 2023 | www.osha.go.tz

# Serikali yaikabidhi osha magari na vifaa vya bilioni 4.3



## Osha tanzania bara na zanzibar kushirikiana kuimarisha usalama na afya kazini. Uk.3

## Naibu waziri awabana wawekezaji wanaokiuka sheria za kazi. Uk.4

## Wawekezaji viwanda waaswa kuzingatia sheria na miongozo ya kazi. Uk5



# Serikali yaikabidhi osha magari na vifaa vya bilioni 4.3

Juni 30, 2023

Waziri wa Nchi Ofisi ya Waziri Mkuu (Kazi, Vijana, Ajira na Wenye Ulemavu), Prof. Joyce Ndalichako ameukabidhi Wakala wa Usalama na Afya Mahali pa Kazi (OSHA) magari 13 na vifaa vya ukaguzi vyenye thamani ya zaidi ya bilioni 2 ambavyo vimetolewa na serikali ili kuboresha utendaji wa Taasisi hiyo.

Magari na vifaa hivyo vyenye thamani ya jumla ya zaidi ya bilioni 4 vimekabidhiwa leo (Juni 30, 2023) katika hafla maalum iliyofanyika katika Ofisi za OSHA zilizopo Kinondoni jijini Dar es Salaam na kuhudhuriwa na menejimenti na watumishi wa OSHA.

Aidha, hafla hiyo ilienda sambamba na ufunguzi wa mafunzo kwa watumishi wapya 18 ambao wameajiriwa ikiwa ni mkakati wa kuendelea kuboresha utendaji wa OSHA.

Akizungumza katika tukio hilo, Waziri Prof. Ndalichako amesema magari na vifaa hivyo vimenunuliwa ikiwa ni utekelezaji wa ahadi ya Rais, Dkt. Samia Suluhu Hassan, aliyoitoa katika maadhimisho ya Mei Mosi mwaka huu yaliyofanyika Kitaifa Mkoani Morogoro ambapo alieleza kuwa serikali yake imepanga kuiongezea hadhi Taasisi ya OSHA

“Haya yote yanafanyika leo ikiwa ni utekelezaji wa ahadi ya Rais wetu mpendwa, Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan aliyoitoa katika hotuba yake akiwa Mgeni Rasmi katika maadhimisho ya Siku ya Wafanyakazi Duniani (Mei Mosi) 2023 yaliyofanyika Kitaifa Mkoani Morogoro. Mheshimiwa Rais aliahidi kununua magari 13 na kuajiri watumishi wapya 18 ili kuiongezea Taasisi ya OSHA uwezo zaidi wa kutekeleza majukumu yake,” **ameeleza Waziri Ndalichako.**




# Osha tanzania bara na zanzibar kushirikiana kuimarisha usalama na afya kazini

Julai 27, 2023

**Ninawashukuru viongozi wa Idara ya Usalama na Afya kwa kutambua kazi nzuri inayofanywa na OSHA kwa upande wa Tanzania Bara katika kusimamia ustawi wa wafanyakazi jambo lililopelekea wao kuja kwetu kujifunza kwa ajili ya kuweza kuchukua yale mazuri yanayoweza kusaidia katika kuleta ustawi wa wafanyakazi kwa hapa Zanzibar**

**Bi. KHADIJA MWENDA**
Mtendaji Mkuu - OSHA

Wakala wa Usalama na Afya Mahali pa Kazi (OSHA) na Idara ya Usalama na Afya Kazini ya Zanzibar wamesaini makubaliano ya mashirikiano katika usimamizi wa masuala ya usalama na afya baina ya pande hizo mbili.

Hafla ya kusaini makubaliano hayo imefanyika Zanzibar na kushuhudiwa na Viongozi mbalimbali wakiwemo: Waziri katika Afisi ya Rais-Kazi, Uchumi na Uwekezaji ya Zanzibar, Mudrik Ramadhan Soraga ambaye ndiye alikuwa Mgeni Rasmi, Katibu Mkuu -Afisi ya Rais-Kazi, Uchumi na Uwekezaji ya Zanzibar, Bi. Maryam Juma Abdulla, Katibu Mkuu katika Ofisi ya Waziri Mkuu-Kazi, Vijana, Ajira na Wenye Ulemavu, Prof. Jamal Katundu na pamoja na Mwenyekiti wa Bodi ya Usimamizi ya OSHA, Dkt. Adelhelm Meru.

Akizungumza katika hafla hiyo, Waziri Soraga amesema makubaliano hayo yatakuwa na nafasi muhimu katika kukuza mashirikiano yaliyokuwepo tangu zamani katika ya OSHA Bara na Zanzibar

Kwa upande wao, Mtendaji Mkuu wa OSHA, Bi. Khadija Mwenda na Mkurugenzi wa Idara ya Usalama na Afya, Dkt. Ali Said Nyanga wameeleza kufurahishwa kwao na hatua hiyo muhimu ya kuingia makubaliano jambo ambalo wanaamini litakuwa na manufaa kwa pande zote mbili.



# Naibu waziri awabana wawekezaji wanaokiuka sheria za kazi

Julai 6, 2023

Naibu Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu (Kazi, Vijana, Ajira na Wenye Ulemavu), Patrobas Katambi, amefanya ziara katika viwanda vya Mkoa wa Dar es Salaam ambapo ameeleza kutoridhishwa na hali ya utekelezaji wa Sheria za Kazi, Usalama na afya pamoja na hifadhi kwa jamii katika baadhi ya viwanda.

Akizungumza mara baada ya kufanya ukaguzi wa mifumo ya usalama na afya na uzingatiaji wa sheria za kazi katika kiwanda cha Colourful Industry Limited kilichopo Buza-Temeke jijini Dar es Salaam kinachozalisha bidhaa za plastiki ikiwemo mifagio na vifungashio, Naibu Waziri Katambi, ameutaka uongozi wa kiwanda hicho kuboresha mazingira ya kazi pamoja na kushughulikia changamoto mbali mbali za wafanyakazi ndani ya siku 14.

“Nimetembelea sehemu mbali mbali za uzalishaji katika kiwanda hiki na kubaini ukiukwaji mkubwa wa taratibu za usalama na afya mahali pa ikiwemo wafanyakazi kutopatiwa vifaa vya kujikinga na vihatarishi vya magonjwa na ajali. Hali ya mazingira ya kazi sio nzuri kuna mzunguko finyu wa hewa na hata mwanga hautoshelezi,” amesema Katambi na kuongeza:

“Aidha kuna ukiukwaji wa haki nyingine za wafanyakazi ikiwemo ujira mdogo, wafanyakazi kulazimishwa kufanya kazi kwa zaidi ya masaa yanayoruhusiwa kisheria bila kupatiwa malipo ya ziada pamoja na kutowasilisha michango ya wafanyakazi katika mifuko ya hifadhi kwa jamii.”

Aidha, Katambi alitembelea kiwanda cha Steel Masters Limited kilichopo Chang’ombe jijini Dar es Salaam kinachozalishaji bidhaa za chuma na kufanya ukaguzi wa maeneo ya uzalishaji pamoja na masuala mengine yanayohusu utekelezaji wa sheria za kazi, usalama na afya na hifadhi kwa jamii.



# Wawekezaji viwanda waaswa kuzingatia sheria na miongozo ya kazi

Juni 20, 2023

Wawekezaji wa sekta ya viwanda wametakiwa kuzingatia sheria na miongozo mbalimbali ya kazi nchini ikiwemo kuboresha mifumo ya usimamizi wa usalama na afya mahali pa kazi ili kuwalinda wafanyakazi dhidi ya athari wanazoweza kuzipata wakiwa kazini.

Wito huo umetolewa na Waziri wa Nchi – Ofisi ya Waziri Mkuu (Kazi, Vijana, Ajira na Wenye Ulemavu) Prof. Joyce Ndalichako wakati wa ziara ya Kamati ya Bunge ya Ustawi na Maenedeleo ya Jamii ya kutembelea viwanda Mkoani Arusha akiambatana na kamati hiyo ili kujionea utekelezaji wa sheria na miongozi mbalimbali ya kazi ikiwemo Sheria Na.5 ya Usalama na Afya Mahali pa Kazi ya Mwaka 2003.

**"Kwanza kabisa tunapenda wawekezaji waje nchini kwa wingi na wanapowekeza basi waendeshe shughuli zao zote kwa kuzingatia sheria mbalimbali za nchi ikiwemo sheria na miongozo mbalimbali ya kazi, huwa tunafurahi sana tunapoona wawekezaji wanatengeneza ajira kwa vijana wetu lakini pia wakiendesha shughuli zao kwa mujibu wa sheria za nchi "**

**PROF. JOYCE NDALICHAKO**

"Tunazo sheria za nchi zinazoelekeza viwanda kujenga miundo mbinu rafiki kwa watu wenye ulemavu, mimi leo nimeshindwa kuingia ndani katika baadhi ya viwanda tulivyotembelea kutokataka na ulemavu wangu wa miguu maeneo mengi yana ngazi naamini kuna wafanyabishara wengi wenye ulemavu ambao pengine wanatamani kuingia katika maeneo ya viwanda na wakashindwa kutokana na miundombinu kutokuwa rafiki kwao hivyo wito wangu kwa wawekezaji wote nchini katika sekta hii ya viwanda waboreshe miundommbinu ili kuwapa fursa wenye ulemavu" alisema Makamu Mwenyekiti wa Kamati ya Bunge ya Ustawi na Maenedeleo ya Jamii, Bi. Riziki Saidi.

# Zaidi Ya Watu 600 Ndani Na Nje Ya Nchi Wanufaika Na Huduma Za OSHA Sabasaba 2023

Juni 28 - Julai 13, 2023




Zaidi ya watu 600 kutoka maeneo mbalimbali ndani na nje ya nchi wamenufaika na huduma kadha wa kadha zinazotolewa na OSHA katika Maonesho ya Kimataifa ya 47 ya Biashara Dar es salaam





Miongoni mwa huduma zilizotolewa na OSHA kupitia maonesho hayo ya Kimataifa ni pamoja na Usajili wa maeneo ya kazi unaofanyika kupitia mfumo wa kimtandao wa wims (workplace information management system), elimu na ushauri wa kitaalam wa masuala ya usalama na afya mahali pa kazi, vipimo vya magonjwa yatokanayo na kazi kwa kutumia vifaa vya kisasa,



Aidha viongozi mbalimbali wa serikali walipata fursa ya kutembelea banda la maonesho la OSHA akiwemo Naibu Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu (Kazi, Vijana, Ajira na Wenye Ulemavu), Patrobas Katambi, Katibu Mkuu Ofisi ya Waziri Mkuu (Kazi, Vijana, Ajira na Wenye Ulemavu), Prof. Jamal Adam Katundu, Kamishina wa Kazi, Bi Suzan Mkangwa, Mkemia Mkuu wa Serikali, Dkt.





# OSHA Yaendelea Kuzifikia Sekta Zisizo Rasmi

Julai 15, 2023

Wakala wa Usalama na Afya Mahali pa Kazi (OSHA) umeendelea na mpango mkakati wake wa kuhakikisha makundi mbalimbali katika jamii yanafikiwa na elimu ya masula ya usalama na afya mahali pa kazi ambapo hivi karibuni imeendesha mafunzo maalum kwa wajasiriamali wadogo wa fani mbalimbali ikwemo kutengeneza samani,batiki,kushona nguo, kuchomelea,fundi mwashi, pamoja na wajasiriamali wanaozalisha na kuuza bidhaa mbalimbali.

Akizungumza na wajasiriamali hao wakati akifunga mafunzo Mtendaji Mkuu wa OSHA, Bi. Khadija Mwenda amewahasa wajasiriamali hao kuzingatia mafunzo waliopata kutoka kwa watalaamu wa OSHA ili kuwa na uzalishaji wenye tija na endelevu

“Siku zote tunasema uwekezaji wa kwanza tunapaswa kuwekeza katika afya na usalama wetu li tuwe na uzalishaji endelevu na wenye tija na sisi kama OSHA kwa kutambua kwamba kundi hili la wajasiriamali watu wengi wamejiajiri hivyo jukumu letu ni kuhakikisha ajira hizi zinalinda usalama na afya wa mfanyakazi,zinakuwa zenye staha na endelevu ndio maana tumetoa mafunzo kwa kundi ili waweze kuwa salama dhidi ya vihatarishi vinavyoweza kuwakumba wakati wakitekeleza majukumu yao” alisema Mtendaji Mkuu.

Kupitia mafunzo hayo wajasiriamali hao walipata fursa ya kujifunza masuala mbalimbali yanayohusu usalama na afya mahali pa kazi ikiwemo kutambua vihatarishi vya ajali na magonjwa na namna ya kukabiliana navyo, matumizi sahihi ya vifaa kinga pamoja na kutoa huduma ya kwanza kwa magonjwa ya dharula

**Nitumie fursa hii kumshukuru sana Mhe.Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa kuridhia na kugharamia mafunzo haya kwa wajasiriamali na hii ni sababu ya upendo pamoja na kuthamini mchango wa wajasiriamali katika maendeleo ya taifa letu.**

**Bi. KHADIJA MWENDA**
Mtendaji Mkuu - OSHA



Waziri wa Nchi – Ofisi ya Waziri Mkuu (Kazi, Vijana, Ajira na Wenye Ulemavu) Prof. Joyce Ndalichako akisalimiana na watumishi wa OSHA mapema baada ya kuwasili katika ofisi za OSHA Dar es Salaam kwaajili ya hafla za kukabidhi magari 13 pamoja na kuwakaribisha watumishi wapya 18 katika taasisi hiyo



Waziri wa Nchi – Ofisi ya Waziri Mkuu (Kazi, Vijana, Ajira na Wenye Ulemavu) Prof. Joyce Ndalichako pamoja na Mtendaji Mkuu wa OSHA, Bi Khadija Mwenda, wakikabidhi sanduku la vifaa vya ukaguzi kwa watumishi wa OSHA



Naibu Waziri – Ofisi ya Waziri Mkuu (Kazi, Vijana, Ajira na Wenye Ulemavu) Mhe. Patrobas Katambi akitoa maelekezo kwa wawekezaji wa kiwanda cha chuma cha Steel Master Limited kuhusu uboreshaji wa mifumo ya usalama na afya katika baadhi ya maeneo ya kiwanda hicho yaliyobainika kuwa na mapungufu.




Mtendaji Mkuu wa OSHA, Bi. Khadija Mwenda akieleza namna ambavyo mashirikiano baina ya OSHA na Idara ya Usalama na Afya ya Zanzibar yatakavyoleta mapinduzi ya kiuchumi nchini kwa kuimarisha usalama na afya za wafanyakazi katika maeneo mbalimbali ya kazi.






Waziri wa Nchi Afisi ya Rais- Kazi, Uchumi na Uwezeshaji, Mhe.Mudrik Ramadhan Soraga



Bi. Khadija Mwenda
Mtendaji Mkuu - OSHA




Prof. Jamal Katundu
Katibu Mkuu OWM






Bi. Getrude Sima
Mwakilishi ILO




Dkt.Ali Said Nyanga
Mkurugenzi - DOSH Zanzibar

**Matukio katika picha hafla ya utiaji saini wa hati ya makubaliano ya mashirikiano baina ya OSHA na Idara ya Usalama na afya kazini Zanzibar.**



Naibu Katibu Mkuu Afisi ya Makamu wa Pili wa Rais, Ndg. Salhina Mwita Ameri (katikati) akipokea maelezo kutoka kwa Mkaguzi wa Afya wa OSHA, Amina Nangu (aliyenyoosha mkono) wakati wa kikao kifupi cha ufunguzi wa ukaguzi wa masuala ya usalama na afya katika Ofisi ya Mkamu wa Pili wa Rais Zanzibar.




Mkaguzi wa Usalama wa Umeme wa OSHA, Mhandisi Maria Ndaskoy akifanya ukaguzi wa mifumo ya umeme katika Ofisi ya Rais – Uchumi na Uwekezaji Zanzibar.



Mkaguzi wa Mazingira ya Kazi wa OSHA, Simon Lwaho akitoa maelekezo ya namna sahihi ya matumizi ya kiti cha egonimia katika Ofisi ya Rais – Uchumi na Uwekezaji Zanzibar.





Mkaguzi wa Afya wa OSHA, Dkt. Edwin Senguo akimfanyia vipimo vya afya Mkurugenzi wa Sera na Utafiti katika Ofisi ya Rais – Uchumi na Uwekezaji, Bi. Mhaza Gharib Juma ikiwa ni miongoni mwa programu zilizotekelezwa na OSHA kama sehemu ya mashirikiano katika masuala mbalimbali ya usalama na afya mahali pa kazi na Idara ya Usalama na Afya Mahali pa Kazi ya Zanzibar.



Vipimo vya magonjwa yatokanayo na kazi kwa watumishi wa Ofisi ya Rais – Uchumi na Uwekezaji Zanzibar.

# TUFUATE KATIKA KURASA ZETU ZA MITANDAO YA KIJAMII

OshaTanzania

OSHA ONLINE TV

www.osha.go.tz

SIMU BURE: 0800110091/2